

## **Changamoto katika Matumizi ya Majina ya Lugha za Kigeni nchini Tanzania: Mtazamo wa Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu**

*Adventina Buberwa<sup>1</sup>*

### **Ikisiri**

Wataalamu mbalimbali wameshughulikia suala la uteuzi wa majina ya watu ndani na nje ya Tanzania. Baadhi ya wataalamu (taz. Nyangaywa, 2013; Madila, 2020) wanaeleza kwamba uteuzi wa majina ya watu nchini Tanzania unakabiliwa na changamoto ya kasumba ya kupendelea majina ya lugha za kigeni kuliko majina ya lugha za asili. Pamoja na kudokezwa kwa suala hilo, tafiti husika hazikujishughulisha na uchunguzi zaidi kuhusu kuweka bayana kiwango cha matumizi ya majina husika na changamoto zinazotokana na matumizi ya majina hayo ya kigeni. Suala hili limechochea raghba ya mtafiti kufanya utafiti wa awali kuhusu kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni katika jamii ya Watanzania, mtazamo wa jamii na changamoto zinazotokana na matumizi ya majina hayo nchini Tanzania. Ili kutimiza azma hiyo, makala hii imeongozwa na Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu ambapo kasumba hiyo ya kupendelea majina ya lugha za kigeni inatazamwa kama matokeo ya lugha za kigeni kukandamiza lugha za asili na kutokana na ukandamizaji huo, fikra za jamii ya Watanzania zimeaminishwa kuwa lugha za kigeni ni bora na zina thamani zaidi kuliko lugha za asili.

### **1.0 Utangulizi**

Kwa mujibu wa Msanjila, Kihore na Massamba (2009), jamiilugha yoyote hujitambulisha kwa kutumia vibainishi mbalimbali ambavyo ni pamoja na utamaduni, mila na desturi, imani, chakula kikuu, mavazi, lugha na uchumi. Wataalamu hawa wanasisitiza kwamba lugha inachukua nafasi kubwa ya kutambulisha jamiilugha inayozungumza lugha husika. Wanaongeza kuwa lugha ya mzungumzaji na utambulisho wake ni mambo mawili yasiyoweza kutenganishwa. Wataalamu hao wanadokeza kwamba jamiilugha yoyote kama haitakuwa tayari kudumisha utamaduni na lugha yake ya asili, ni wazi kwamba utambulisho wa jamiilugha hiyo unaweza kupotea. Imefafanuliwa kuwa lugha ya asili hubeba amali za jamii inayozungumza lugha husika. Pamoja na ukweli huu, suala la uteuzi wa majina kutoka katika lugha za kigeni kwa jamiilugha mbalimbali nchini Tanzania limeendelea kushamiri kama ilivyobainishwa katika tafiti mbalimbali (Nyangaywa, 2013; Buberwa, 2017; na Madila, 2020.

---

<sup>1</sup> Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Barua pepe: buberwaadventina@yahoo.com

Kutokana na changamoto hii, makala hii inaangazia kiwango cha matumizi ya majina yanayotokana na lugha za kigeni na changamoto zinazotokana na matumizi ya majina hayo na mtazamo wa watoataarifa kuhusu matumizi ya majina ya lugha za kigeni nchini Tanzania. Kwa kufanya hivyo, makala inaonesha mwelekeo wa jamii ya Watanzania kuhusiana na suala la kuthamini, kukuza na kuendeleza lugha za asili na utamaduni kwa ujumla.

## **2.0 Muhtasari wa Mapitio ya Maandiko kuhusu Utoaji wa Majina ya Watu**

Kipengele cha majina ya watu kimeshughulikiwa na wataalamu mbalimbali. Kwa mfano, Rubanza (2000) alichunguza majina ya watu kwa kuzingatia michakato ya kimofolojia inayohusika katika kuunda majina ya watu yanayotokana na lugha ya Kihaya. Katika makala hiyo, anaeleza kwamba majina ya watu yanaweza kuainishwa katika makundi matatu ambayo ni majina yasiyonyambulishwa, majina yaliyonyambulishwa na majina ambatani. Zaidi ya hayo, makala inaangazia masuala mbalimbali yaliyochochea uteuzi wa majina ya Kihaya. Masuala yaliyobainishwa ni pamoja na migogoro ya kifamilia, hali ya mama na mtoto wakati wa kujifungua, mpangilio wa watoto kwa kuzaliwa na maumbile ya mtoto husika.

Nao Carpusor na Loges (2006) walifanya uchunguzi kuhusu athari ya majina katika kupata nafasi ya kupangisha chumba au nyumba mjini Los Angeles. Wataalamu hawa wanaeleza kwamba maombi yaliyowasilishwa yakiwa na majina yaliyofanana na majina ama ya Kiafrika au Kiarabu hayakupewa kipaumbele. Aidha, majina yaliyoonekana kufanana na majina ya Kizungu yalipewa kipaumbele zaidi katika kupewa nafasi za kupata nyumba za kupanga nchini humo. Matokeo ya andiko hilo yanadhihirisha kwamba jina la mtu hudokeza nafasi yake kijamii, historia yake na mahusiano yake ya kikabila.

Kwa upande wa Massamba (2009), Abdul (2013) na John (2016), wanaeleza kwamba majina ya watu hudokeza maana mbalimbali ambazo hutokana na utamaduni wa jamii inayozungumza lugha husika. Pia, wataalamu hao wanaeleza kuwa kuna sababu zinazochochea utoaji wa majina ya watu na miongoni mwa sababu wanazozitaja ni suala la imani za kidini, mila na desturi, kigezo cha muda, namna mtoto alivyozaliwa, mahusiano ya wazazi, mwonekano wa watu, na tabia ya mtoto.

Naye Nyangaywa (2013) ameangazia maana za majina ya Kijita, sababu, taratibu na changamoto zinazokabili utoaji wa majina katika jamii ya Wajita. Miongoni mwa changamoto zilizobainishwa ni pamoja na wanajamii kupendelea majina yanayotokana na lugha za kigeni. Imefafanuliwa zaidi kwamba hata watoto wakipewa majina ya asili huwa hayatumiki kama yale ya lugha za kigeni. Kwa msingi huo, makala hii ya sasa inalenga kuchunguza suala la matumizi ya majina ya kigeni kwa vijana wanaotoka katika jamiilugha mbalimbali za Tanzania ili kubaini kiwango cha matumizi ya majina hayo kisha kubainisha na kufafanua changamoto zinazotokana na suala hilo.

Kwa upande mwingine, Buberwa (2017) amechunguza majina ya watu yanayotokana na lugha ya Kiswahili. Lengo la makala hiyo lilikuwa kufafanua masuala ya kiisimujamii yaliyochochea uteuzi wa majina ya Kiswahili na kutathmini kama masuala hayo yanafahamika kwa wenye majina husika. Matokeo ya uchunguzi huo yanaonesha kwamba wanajamii wengi hususani vijana hawajui maana za majina yao. Imefafanuliwa zaidi kwamba hali hiyo inatokana na matumizi ya majina ya lugha za kigeni ambayo hata wazazi wao hawakutambua maana yake. Kwa kuzingatia matokeo hayo, makala hii ya sasa inalenga kuchunguza changamoto zinazotokana na matumizi ya majina ya kigeni ili kubainisha changamoto zinazotokana na matumizi ya majina hayo.

Buberwa (2019) amechunguzwa majina ya watu yanayotokana na lugha ya Kihaya. Katika utafiti wake amedokeza kukosekana kwa usawa baina ya majina ya watoto wa kiume na majina ya watoto wa kike ambapo anaeleza kwamba majina ya watoto wa kiume yanaibua dhana ya umaarufu wa watoto wa kiume ilhali majina ya watoto wa kike yakirejelea masuala ya mapenzi, ndoa na urembo. Anahitimisha kwamba uteuzi wa majina katika jamii ya Wahaya unaibua ubaguzi na anapendekeza kwamba ni vyema jamii kuteua majina ambayo hayataleta mgawanyiko wa kijamii ili kujenga jamii yenye umoja na mshikamano. Andiko hili halikugusia masuala ya uteuzi wa majina ya kigeni kwa kuwa halikuwa lengo la makala husika.

Tofauti na Buberwa (2019), Madila (2020) amechunguza matumizi ya Kiswahili katika utoaji wa majina ya watu jijini Dar es Salaam. Utafiti huo wa kitakwimu umebainisha kwamba kiwango cha matumizi ya Kiswahili katika utoaji wa majina ya Kiswahili ni asilimia 26.25 ilhali kiwango cha lugha zingine zikiwamo za kigeni kikiwa ni asilimia 73.75 ya majina yote yaliyochunguzwa. Kwa kuwa halikuwa lengo la mtafiti kubainisha kiwango cha matumizi ya majina yanayotokana na lugha za kigeni, suala hilo halikuwekwa bayana. Hata hivyo, mtafiti ameeleza masuala mbalimbali yanayoathiri matumizi ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na kasumba ya jamii kupenda majina yanayotokana na lugha za kigeni. Kwa kuzingatia hali hiyo, makala hii inachunguza kiwango cha matumizi ya majina yanayotokana na lugha za kigeni kwa vijana wanaosoma Shahada ya Kwanza katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kubainisha hali ilivyo katika jamii pana ya Kitanzania na kuchunguza athari zinazotokana na hali hiyo.

Wataalamu wengine waliochunguza majina ya watu ni Lusekelo na Mtenga (2020). Wao wameshughulikia jinsi historia ya jamii za Kiafrika inavyoakisiwa katika majina ya watu. Utafiti huo umefanyika mkoani Kilimanjaro na umehusisha jamii ya Wachaga waishio Rombo. Katika makala hiyo imeelezwa kwamba mchakato wa utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wachaga umeathiriwa na Uislamu, Ukristo na ukoloni. Imeongezwa kuwa majina ya Kichaga hutokana na ama misingi ya kidini au lugha za kigeni kama Kiingereza na Kiswahili. Kwa hiyo, katika makala hiyo Kiswahili kimechukuliwa kuwa lugha ya kigeni kwa jamii ya Wachaga. Hata hivyo, suala hili linahitaji kuchunguzwa zaidi ili kujiridhisha ikiwa

lugha hiyo ina sifa ya kurejelewa kama lugha ya kigeni kwa kuwa lugha ya Kiswahili kwa jamii nyingi za Kitanzania inaonekana kuwa lugha ya pili kwa wazungumzaji walio wengi. Kwa upande wa makala hii ya sasa, lugha ya Kiswahili haitahusishwa katika lugha za kigeni. Lugha zitakazohusishwa ni zile ambazo si za asili nchini Tanzania. Lugha hizo ni Kiingereza, Kichina, Kiarabu, Kijerumani na Kifaransa.

Nao Lusekelo na Mtenga (2020) wamechunguza jinsi historia ya jamii za Kiafrika inavyoakisiwa kwenye majina ya watu. Utafiti huo ulifanyika Kilimanjaro na ulihusisha Wachaga waishio Rombo. Andiko hilo linaeleza kwamba mchakato wa utoaji wa majina katika jamii ya Wachaga umeathiriwa na Uislamu, Ukristo na ukoloni. Aidha, ilifafanuliwa kwamba majina hayo hutokana na misingi ya kidini au lugha za kigeni ambapo lugha hizo zinarejelewa kuwa ni Kiingereza na Kiswahili. Kwa kuzingatia hoja hii, ni kwamba lugha ya Kiswahili inachukuliwa kuwa lugha ya kigeni kwa sababu si lugha ya kwanza kwa jamii ya Wachaga. Kwa mujibu wa makala hii ya sasa, lugha ya kigeni inachukuliwa kuwa ni ile ambayo asili yake ni nje ya Tanzania. Hivyo basi, lugha ya Kiswahili inachukuliwa kuwa lugha ya asili.

Pia, Anthony (2021) amechunguza majina ya dawa za asili ili kufafanua maana zake na masuala ya kiisimujamii yanayochochea uteuzi wa majina hayo. Katika utafiti huo, amegusia kipengele cha majina ya watu ambapo ameeleza kuwa baadhi ya majina ya dawa za asili hutokana na majina ya watu ambao ndio wamiliki au wagunduzi wa dawa husika. Kwa kuwa andiko hili lilihusu majina ya dawa za asili, kipengele cha majina ya watu hakikushughulikiwa kwa kina zaidi. Kipengele hiki ndicho kinachochunguzwa katika makala hii ambapo kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni na changamoto zitokanazo na matumizi ya majina hayo vimewasilishwa.

Aidha, Kimbwanda (2021) ameangazia kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za asili yanayorejelea watu. Lugha zilizohusishwa ni Kiswahili na Kingindo kwa lengo la kuchunguza kiwango cha matumizi ya lugha hizo katika utoaji wa majina ya watu katika jamii ya Wangindo. Matokeo ya utafiti huo pamoja na masuala mengine, yamedokeza kwamba asilimia 95 ya watoataarifa vijana waliohusishwa walipendekeza majina ya Kiarabu yatumike zaidi kwa sababu yanaambatana na dini yao tukufu ya Kiislamu. Hoja hii imemchochea mtafiti kuchunguza majina ya vijana wanaotoka katika jamii mbalimbali kwa lengo la kubaini suala la matumizi ya majina ya kigeni linajibainisha vipi kwa vijana hao ili kupata matokeo yenye mawanda mapana kuhusu kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni kwa jamii ya Watanzania na changamoto zake kwa jamii husika.

Kwa ujumla, maandiko yaliyopitiwa yanaonesha kwamba jamii hutumia majina ya watu na majina hayo yana maana, sababu, na masuala ya kiisimujamii yanayochochea uteuzi wa majina hayo. Pia, majina hayo huwatambulisha wanajamii wenye majina husika. Hata hivyo, katika baadhi ya maandiko

imebainika kwamba uteuzi wa majina ya watu nchini Tanzania unakabiliwa na changamoto ya kasumba ya kupendelea majina yanayotokana na lugha za kigeni. Changamoto hii imebainishwa katika jamii kadhaa ikiwa ni pamoja na jamii za Wangindo na Wajita. Suala hili limeonekana kujitokeza zaidi kwa kundi la vijana kuliko kwa watu wazima na wazee. Kwa msingi huu, makala hii inachunguza kiwango cha matumizi ya majina ya watu yanayotokana na lugha za kigeni kwa vijana wanaotoka katika jamiilugha mbalimbali za Tanzania ili kupata matokeo jumuiifu. Aidha, makala hii inakwenda mbele zaidi kuangazia changamoto zinazotokana na matumizi ya majina ya lugha za kigeni kwa jamii ya Watanzania.

### **3.0 Mbinu za Ukusanyaji wa Data**

Data ya makala hii imekusanywa kutoka uwandani ambapo watoataarifa kutoka katika jamiilugha 10 za Tanzania wamehusishwa. Jamiilugha hizo ni pamoja na Wasukuma, Wabena, Wanyakyusa, Wajita, Wachaga, Wangindo, Wazaramo, Wakinga, Wahaya na Wasambaa. Jamiilugha hizi ziliteuliwa kinasibu kwa kuwa jamiilugha yoyote iliyopo nchini Tanzania ingeweza kushirikishwa katika utafiti huu ili kuwakilisha jamiilugha za Tanzania. Watoataarifa walioshiriki walikuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza hadi wa tatu, wa shahada ya kwanza ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanaosoma kozi za Kiswahili, wenye umri kati ya miaka 20–25 kwa mwaka wa masomo 2019/2020. Kuteuliwa kwa kundi hilo kumetokana na malengo ya makala husika ya kuchunguza majina ya kwanza ya vijana ili kubainisha ni kwa kiasi gani majina waliyonayo yanatokana na lugha za kigeni kama tafiti za awali zinavyoeleza. Hivyo basi, uteuzi huo ulifanywa kwa kuzingatia mbinu ya usampulishaji kusudio ili kupata watoataarifa waliokusudiwa pekee.

Aidha, uteuzi wa sampuli ulifanywa kwa mbinu ya usampulishaji nasibu taratibishi ambapo wanafunzi kutoka katika jamiilugha teule walipatikana katika madarasa matano na katika kila darasa waliteuliwa wanafunzi wanaotoka katika jamiilugha mbili pekee. Wanafunzi wa jamiilugha moja, wenye umri uliobainishwa, waliombwa kukutana na mtafiti baada ya kipindi kisha wale ambao walikuwa wa kwanza kuhesabu namba 1 - 10 ndio waliohusishwa kwenye utafiti huu. Hivyo basi, jumla ya watoataarifa 20, ambao 10 walitoka katika kila jamiilugha moja walipatikana katika kila darasa na kufanya jumla ya watoataarifa wa makala hii kuwa 100. Data iliyokusanywa ni pamoja na majina yao ya kwanza na maoni yao kuhusu majina hayo. Data hiyo ilikusanywa kwa mbinu za usaili na hojaji ambapo watoataarifa wote walisailiwa kisha kujaza hojaji fupi kuhusu taarifa za majina yao. Data iliyokusanywa kwa mbinu ya usaili ilirekodiwa kwa kutumia simu. Mbinu mbili za ukusanyaji wa data zilihusishwa kwa sababu mtafiti alilenga kupata majina husika katika tahajia zake halisi na ufafanuzi kuhusu majina hayo ulifaa sana kupatikana kwa njia ya mahojiano ya ana kwa ana ili kubaini mitazamo ya watoataarifa katika muktadha halisi.

Zaidi ya hayo, uchanganuzi wa data ulifanywa kwa mikabala ya kitaamuli na kitakwimu. Katika mkabala wa kitaamuli, mtafiti ametumia mbinu ya ethnografia ambayo huhusisha kuchunguza utamaduni wa jamii au kundi fulani kwa kuangazia masuala mbalimbali yakiwamo lugha, imani, taratibu na mitazamo ya jamii inayochunguzwa (Gary na Mahoney, 2012). Kwa kutumia mbinu hiyo, mtafiti ameshughulikia majina yaliyokusanywa kwa kuyahusianisha na changamoto zinazotokana na matumizi ya majina hayo katika maendeleo ya utamaduni wa jamiilugha ya Watanzania. Kwa upande wa mkabala wa kitakwimu, mbinu wiani imetumika. Hii ni mbinu ambayo hutumika kuchunguza kiwango cha uhusiano baina ya vigeu viwili au zaidi. Kwa kutumia mbinu hiyo, mtafiti amechunguza kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni na lugha za asili ili kuweka bayana ikiwa majina ya lugha za kigeni yanatumika zaidi kuliko majina ya lugha za asili. Hivyo basi, kiwango kimewasilishwa kwa kukokotoa takwimu za majina yaliyotumika kisha kuwasilisha takwimu hizo kwa viwango vya asilimia. Vigeu vilivyohusishwa vimegawanyika katika makundi mawili ambayo ni majina ya kigeni na ya kiasili. Kipengele kinachofuata kinaangazia mkabala wa kinadharia ulioongoza uchanganuzi wa data za makala hii.

#### **4.0 Mkabala wa Kinadharia**

Uchanganuzi wa data za makala hii umeongozwa na Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu iliyoasisiwa na Phillipson (1992). Nadharia hiyo inahusu hali ya lugha moja yenye nguvu kisiasa na kiuchumi kukandamiza lugha isiyo na nguvu. Hii ina maana kwamba lugha yenye nguvu hupendelewa na kupewa nafasi zaidi katika matumizi ilhali nafasi ya lugha isiyo na nguvu katika matumizi ikiminywa. Nadharia hii ina mihimili mikuu minne ambayo ni mfumo kandamizi, mitazamo, kusukumwa kwa lugha zingine na kupingwa. Licha ya kuwapo kwa mihimili hiyo, makala hii imeongozwa na mihimili miwili pekee ambayo ni mhimili wa mfumo kandamizi na mhimili wa mitazamo. Mihimili hii imeteuliwa kwa sababu makala hii inajenga msingi kuwa, hali ya jamiilugha ya Watanzania kupendelea majina ya kigeni kuliko majina ya asili inatokana na mfumo kandamizi ambapo lugha zenye nguvu (lugha za kigeni) zinakandamiza lugha zisizo na nguvu (lugha za kiasili). Pia, hali hiyo inafungamana na mtazamo wa jamii ya Watanzania kwamba wameaminishwa kuwa lugha kandamizi ni bora kuliko lugha zao za kiasili. Kwa kutumia mihimili hiyo, mtafiti amechunguza kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni, mtazamo wa watoataarifa kuhusu majina ya lugha za kigeni na changamoto zinazotokana na matumizi ya majina hayo. Kwa ujumla, nadharia teule imeongoza vyema uchanganuzi wa data za makala hii.

#### **5.0 Kiwango cha Matumizi ya Majina ya Lugha za Kigeni**

Lengo mojawapo la makala hii lilikuwa ni kuchunguza kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni ambapo jina lililoshughulikiwa ni la kwanza la kila mtoataarifa aliyehusishwa katika utafiti huu. Kama ilivyoelezwa awali katika

kipengele cha 3.1 cha makala hii, data za kipengele hiki zilikusanywa kwa njia ya usaili ambapo watoatarifa walitakiwa kutaja majina yao ya kwanza na kubainisha majina hayo ni ya lugha za kigeni au lugha za kiasili. Watoatarifa walioshiriki walikuwa 100 na matokeo kuhusu kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni yalikuwa kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 1: Kiwango cha Matumizi ya Majina ya Lugha za Kigeni**

Jamiilugha Teule	Idadi ya Jumla ya Majina Yaliyokusanywa	Idadi ya Majina ya Lugha za Kigeni	Idadi ya Majina ya Lugha za Asili	Lugha Zilizohusika
Wasukuma	10	7	3	Kisukuma, Kiingereza, Kiebrania
Wabena	10	7	3	Kiingereza, Kibena, Kiswahili
Wajita	10	9	1	Kiingereza, Kijita
Wahaya	10	8	2	Kiingereza, Kiswahili, Kihaya
Wanyakyusa	10	8	2	Kiingereza, Kinyakyusa
Wakinga	10	7	3	Kiingereza, Kikinga
Wazaramo	10	7	3	Kiingereza, Kiarabu, Kiswahili
Wangindo	10	7	3	Kiingereza, Kiarabu, Kiswahili, Kingindo
Wachaga	10	8	2	Kiingereza, Kichaga
Wasambaa	10	7	3	Kiingereza, Kiarabu, Kisambaa
JUMLA	100	77	22	
%	100%	77%	23%	

**Chanzo:** Uwandani (2019/2020)

Kama data katika Jedwali Na. 1 inavyoonesha, kiwango cha matumizi cha majina ya kwanza yanayotokana na lugha za kigeni kiko juu tukilinganisha na kiwango

cha majina yanayotokana na lugha za asili. Kwa kuzingatia Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu, ni wazi kwamba lugha za kigeni zimekandamiza lugha za asili ambapo jumla ya majina 77 (77%) kati ya majina 100 (100%) yametokana na lugha za kigeni. Hali hii inaweka wazi kwamba tamaduni za Kiafrika na historia ya jamiilugha husika vinaendelea kukandamizwa na tamaduni za kigeni. Matokeo haya yanaonesha kuwapo kwa watu wengi wanaoendeleza lugha na historia ya mataifa ya kigeni. Matokeo haya yanaibua dukuduku ikiwa uhuru wa nchi huru na watu wake ni halisi au ni matamko tu ilhali jamii ikiendelea kutawaliwa kifikra.

### **6.0 Changamoto Zinazotokana na Matumizi ya Majina ya Lugha za Kigeni**

Sehemu hii inaangazia changamoto zitokanazo na matumizi ya majina ya lugha za kigeni. Kama ilivyoelezwa awali katika kipengele cha 2.0 cha makala hii, data za kipengele hiki zilikusanywa kwa kutumia mbinu mbili za ukusanyaji wa data ambazo ni usaili na hojaji. Majina yaliyokusanywa yamechanganuliwa kwa kubainisha changamoto zilizojibainisha kutokana na matumizi ya majina hayo ya lugha za kigeni. Changamoto husika zimejadiliwa katika sehemu zinazofuata.

### **6.1 Baadhi ya Majina ya Lugha za Kigeni ni Magumu Kutamkwa**

Kutokana na data za majina yaliyokusanywa kwa njia ya hojaji na usaili, imebainika kwamba majina mengi ya watoataarifa walioshiriki yanatokana na lugha za kigeni. Aidha, baadhi ya watoataarifa walieleza kwamba changamoto wanayokumbana nayo ni ugumu wa kutamka majina yao hususani kwa jamii inayowazunguka. Ifuatayo ni mifano ya majina yaliyobainishwa na watoataarifa:

### **Jedwali Na. 2: Mifano ya Majina ambayo baadhi ya Watu Hushindwa Kuyatamka Ipasavyo**

<b>Na.</b>	<b>Jina Halisi</b>	<b>Jina Lililorahisishwa</b>
1.	Arbogast	Ali
2.	Bernardo	Belena
3.	Adalberta	Adi
4.	Nicholaus	Ndikola
5.	Cephas	Sefu
6.	Fairness	Fenesi

**Chanzo:** Uwandani (2019/2020)

Majina yaliyoorodheshwa kwenye safu ya ‘jina halisi’ yalibainishwa na watoataarifa katika hojaji walizopewa. Hata hivyo, watoataarifa hao waliongeza ufafanuzi kwamba kutokana na changamoto ya kushindwa kutamka majina hayo, baadhi ya ndugu, walezi na watu wao wa karibu huwarejelea kwa majina yaliyobainishwa kwenye safu ya ‘jina lililorahisishwa’. Mtoataarifa mmoja alinukuliwa akieleza hivi wakati wa usaili:

Mimi kama mimi jina langu ni *Nicholaus* lakini kwa sababu ya baadhi ya watu kushindwa kutamka jina hilo, huniita *Ndikola* na ni jina ambalo limezoeleka sana nyumbani kwetu. Hivyo, wakati mwingine wanapoandika orodha ya majina huandika jina la *Ndikola* badala ya *Nicholaus* ...

Kwa kuzingatia data hii, ni wazi kwamba majina yanayotokana na lugha za kigeni wakati mwingine huwa ni magumu kuyatamka hususani kwa baadhi ya wanajamii ambao hawawezi kuzungumza lugha za kigeni. Kutokana na ugumu huo, jamii hujaribu kutafuta njia rahisi ya kumrejelea mhusika, jambo ambalo huwafanya kuibuka na jina jipya ambalo linaweza kuwa tofauti kabisa na jina halisi. Kwa mfano, jina namba 6 katika Jedwali Na. 2 unaweza kudhani ni jina la Kiswahili linalorejelea tunda ambalo ni *fenesi* ilhali ni jina lililotokana na majaribio ya kurahisisha matamshi ya jina halisi *Fairness*. Hivyo basi, ni bayana kuwa jamii inatumia majina ambayo wakati mwingine haiwezi kuyatamka; ni vigumu kujua ni majina ya jamiilugha ipi na yanatambulisha lugha ipi. Pamoja na changamoto hii, jamii inaamini kwamba majina ya lugha za kigeni ni bora zaidi kuliko ya asili. Suala hili linaenda pamoja na mhimili wa mitazamo katika Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu unaodai kwamba mtumiaji wa lugha kandamizwa hugeuzwa fikra na kuona kwamba lugha yake ni dhaifu na badala yake lugha kandamizi huonekana ina nguvu na inamfanya yeye aonekane ana nguvu. Kwa hakika huu ni ubeberu wa kiisimu unaotawala fikra za jamiilugha inayopendelea lugha za kigeni kuliko lugha zake ya asili.

## 6.2 Baadhi ya Majina ya Lugha za Kigeni Yanayotumika Yana Makosa ya Kitahajia

Baada ya kuchunguza majina ya watoataarifa yaliyoandikwa kwenye hojaji walizozijaza, imebainika kwamba baadhi ya majina ya wahusika yalikuwa na makosa ya kitahajia. Mifano ya majina hayo ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3 lifuatalo:

### Jedwali Na. 3: Mifano ya Majina yenye Makosa ya Kitahajia

Na.	Jina lenye Makosa ya Kitahajia	Jina Sahihi
1.	Lytines	Lightness
2.	Inocent	Innocent
3.	Jacline	Jacqueline
4.	Pascal	Paschal

**Chanzo:** Uwandani (2019/2020)

Mifano katika Jedwali la 2 inadhihirisha kwamba baadhi ya majina yaliyobainishwa na watoataarifa kuwa ni ya lugha ya Kiingereza, yalikuwa na makosa ya kitahajia. Wakati wa usaili, watoataarifa hao walithibitisha kwamba

majina yao ya kwanza huandikwa kama yalivyoorodheshwa kwenye safu ya *jina lenye makosa ya kitahajia* na ndivyo yalivyoandikwa katika nyaraka muhimu kama vyeti vya kuzaliwa na vyeti vya kuhitimu masomo ya ngazi mbalimbali. Ili kujiridhisha kama majina husika yalilengwa kuwa ya Kiingereza, mtafiti aliuliza maana za majina husika. Watoataarifa wote walibainisha maana halisi za majina sahihi ya Kiingereza ijapokuwa majina yao yalikuwa na makosa ya kitahajia. Hivyo basi, jamii inateua majina ya lugha za asili kuyafanya majina ya utotoni na ya utani ilhali majina ya lugha za kigeni yasiyofahamika vyema na yenye makosa ya aina hii yanateuliwa kuwa majina rasmi ya kutumika katika maeneo rasmi. Kwa kuzingatia Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu, lugha ya Kiingereza imekandamiza lugha za asili ambapo imepata upendeleo wa kutumika hadi kwenye vipengele muhimu vya utambulisho wa kijamii kama vile majina ya watu wa jamii ya Watanzania. Huu ni utumwa wa kifikra na kimtazamo ambapo jamii inajiona dhaifu na amali zake pia. Hivyo, kutumia majina ya lugha za kigeni ni kujaribu kupandisha hadhi ya jamiilugha husika. Makala hii inatoa wito kwa jamii kujitafakari upya kuhusu suala hili ili jamii iwe na hamasa ya kutunza na kuendeleza utamaduni wake badala ya kuteua majina isiyoyajua tahajia zake kwa lengo la kujiambatanisha na jamiilugha za kigeni.

### **6.3 Baadhi ya Majina ya Lugha za Kigeni Yanayotumika Hujitokeza katika Maumbo Zaidi ya Moja**

Baadhi ya majina yaliyokusanywa kutokana na mbinu ya hojaji yamebainika kuwa ni jina moja lenye umbo zaidi ya moja. Moja miongoni mwa majina yaliyokuwa na maumbo zaidi ya moja ni hili lifuatalo:

#### **Jedwali Na. 4: Jina Moja lenye Maumbo Zaidi ya Moja**

<b>Idadi ya Maumbo</b>	<b>Jina Linalohusika</b>
Umbo la kwanza	Emanuel
Umbo la pili	Emmanueli
Umbo la tatu	Emmanuel
Umbo la nne	Immanuel
Umbo la tano	Emmanuely

**Chanzo:** Uwandani (2019/2020)

Kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4, ni wazi kwamba jina ni moja lakini linajibainisha katika maumbo tofauti. Watoataarifa wote walibainisha maana ya jina hilo inayofanana wakati wa usaili. Walieleza kwamba walizaliwa ama wakati wa sikukuu ya Noeli au siku chache kabla au baada ya sikukuu hiyo. Suala la kushangaza ni kwamba licha ya kuwapo kwa jina lenye tahajia za Kiswahili ambalo ni *Immanueli* linalopatikana katika Biblia Takatifu (taz. Mathayo 1:23),

imebainika kwamba jamii inatafuta kwenda na usasa wa kutumia majina ya lugha za kigeni. Utashi wa kutaka kutumia majina ya lugha zisizojulikana vyema kwa jamii husika unasababisha kuwa na maumbo mbalimbali yanayokusudiwa kuwa jina lilelile moja. Baadhi huwa na makosa na hupoteza asili ya jina husika kama mfano wa umbo la pili *Emmanueli* unavyodhihirika. Jina hilo linaonekana kuwa na mwelekeo wa kuwa lugha ya Kiswahili lakini mfuatano wa konsonanti mbili unavuruga ruwaza ya silabi za Kiswahili. Vurugu ya jinsi hii ni matokeo ya ubeberu wa kiisimu ambapo jamii inakumbwa na upepo wa kutawaliwa kifikra na kintazamo kutokana na lugha za kigeni zinazotumiwa na mataifa yenye uchumi wenye nguvu, siasa na utawala wenye nguvu. Hatimaye, lugha za jamiilugha hizo huwa na nguvu; hivyo kukandamiza lugha za jamiilugha zisizo na nguvu. Kwa ujumla, mihimili teule ya Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu inashikamana vyema na matokeo haya kwa kuwa lugha za kigeni zinaonekana kukandamiza lugha za asili na fikra za jamiilugha kandamizwa zinaonekana kukubaliana na wazo kwamba lugha yake ni dhaifu ilhali lugha za kigeni ni bora na zina nguvu.

#### **6.4 Majina ya Lugha za Kigeni Yakitumika Hupoteza Dhima yake ya Utambulisho wa Jamii**

Baada ya kuchunguza data ya majina yaliyokusanywa kwa njia ya hojaji, imebainika kwamba majina kama *Paschal, Innocent, Godlove, Charles, Quinter, Happiness, Dominick* na *Dickson* yanaibua wazo kwamba huenda wenye majina hayo ni watu kutoka jamiilugha zinazopatikana katika bara la Ulaya ilhali wao ni Watanzania ambao wakati mwingine hata lugha mojawapo ya Ulaya hawajawahi kuizungumza. Hali hii ni hatari kwa maendeleo ya lugha na utamaduni wa Mtanzania. Kwa kufanya hivyo, Mtanzania anatambulisha jamii ya kigeni badala ya kutambulisha jamii yake. Suala hili linarejelewa na Giles na Byrne (1982) kwamba jamiilugha inayoacha lugha yake ya asili na kujiungamanisha na lugha ya kigeni huwa haithamini lugha na utamaduni wake. Hivyo, kuendelea kutumia lugha ya kigeni ni suala linalodhoofisha lugha na utamaduni wa jamii husika. Kwa mfano, mtoataarifa mmoja wa data za makala hii, alieleza kwamba alipewa jina la *Michael Jackson* kwa sababu baba yake alikuwa mwanamuziki na alimpenda sana Marehemu Michael Jackson. Kwa ujumla, uteuzi wa majina ya watoto ni suala linalohitaji kuchukuliwa kwa umuhimu sana kwa kuwa majina ya watu yakitokana na lugha za jamii husika hubeba historia ya jamii husika, amali za jamii na utamaduni kwa ujumla.

#### **6.5 Majina ya Lugha za Kigeni Huhifadhi na Kuendeleza Historia ya Jamii za Kigeni**

Katika uchunguzi wa majina yaliyokusanywa kwa ajili ya makala hii, imebainika kwamba majina ya kigeni hayahifadhi historia na utamaduni wa jamii ya mwenye jina. Imebainika kwamba majina machache yanayotokana na lugha za kigeni yanadokeza mambo ya kufurahisha, kutuliza au kutia moyo, upendo na imani kwa

Mungu mmoja na shukurani. Majina ya watu yana dhima kubwa ya kuhifadhi historia ya jamii inayozungumza lugha husika (Msanjila, 2009; Lusekelo na Mtenga, 2020). Jambo hili halijitokezi pale jamii inapoamua kutumia majina ya kigeni. Majina hayo, hujengwa katika msingi wa historia za jamii za kigeni ambapo historia ya jina lenyewe hurejelea masuala ambayo kwa hakika hayamhusu mwenye jina na jamii yake. Kwa mfano, baadhi ya watoataarifa walioshiriki katika utafiti huu walieleza kwamba walipewa majina yao ya kwanza kutokana na mahitaji ya kidini kwamba majina yao sharti yatokane na Maandiko Matakatifu.

Kutokana na hitaji hilo, mmoja wao aliyeitwa *Nicholaus* aliripoti kwamba babu yake alimwambia kwamba jina hilo lina maana ya “ushindi wa watu”. Aliendelea kueleza kwamba jina hilo linahusishwa na Mtakatifu *Nicholas* ambaye alikuwa Askofu wa Kigiriki wa Karne ya Nne. Taarifa hizi zinabainisha kwamba historia inayohusishwa na jina husika inahusu jamii ya kigeni na si jamii ya mwenye jina. Hii ina maana kuwa vizazi vijavyo vikapohitaji kupata taarifa kuhusu majina ya ama baba na mama au babu na bibi, ufafanuzi utakaotolewa ni wa aina hiyo. Ufafanuzi huo utaendeleza historia ya jamii za kigeni ilhali utamaduni wa Mwafrika wa asili ukiendelea kudhoofika. Suala hili linashabihiana na mhimili wa Nadharia ya Ueberer wa Kiisimu kwa kuwa ni wazi kwamba historia, amali za jamiilugha husika zinakandamizwa wakati zile za kigeni zinaendelea kupewa nafasi. Hali hii inatokana na kwamba jamii imeaminishwa kuwa lugha za kigeni ni bora zaidi kwa kuwa zina nguvu kuliko lugha za asili kama mhimili wa mitazamo unavyoeleza. Ili kuepuka changamoto hii, ni vyema jamii zetu kuwa na mtazamo-tofauti na huu uliopo sasa. Badala ya kuwapa watoto majina ya lugha za asili yanayotumika kama majina ya utani au ya utotoni ambayo mara nyingi hayatumiki au husahaulika, ni vyema kuyafanya majina hayo kuwa ya kwanza kwa watoto hao. Hakika ni jambo lisilo na tija pale ambapo jamii inakumbatia majina ya kigeni ilhali majina yake ya asili yanafanywa kuwa ya utani.

### **7.0 Mtazamo wa Vijana kuhusu Matumizi ya Majina ya Lugha za Kigeni**

Utambulisho wa mtu au jamii umefungamana na mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na lugha inayozungumzwa na mtu au jamii husika. Aidha, msingi mwingine unaoweza kumtambulisha mzungumzaji wa lugha fulani ni kujiona kuwa yeye ni sehemu ya jamiilugha yake na ana dhamana ya kuendelea kutumia na kudumisha lugha yake (Tabouret-Killer, 1989). Kwa kuzingatia data iliyokusanywa kwa ajili ya makala hii, kutokana na swali lililoulizwa kwamba, ungependa kutumia majina yapi kati ya majina ya lugha za asili na ya lugha za kigeni kuwa jina lako la kwanza, watoataarifa 81 (81%) kati ya 100 (100%) waliosailiwa walipendekeza majina ya kigeni ilhali watoataarifa 19 (19%) walipendekeza kwamba majina ya lugha za asili yatumike. Tazama data katika Jedwali Na. 5 lifuatalo:

*Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), Juni 2022*

**Jedwali Na. 5: Mtazamo wa Vijana kuhusu Majina ya Lugha za Kigeni na Majina ya Lugha za Asili**

Jamiilugha Teule	Jumla ya Watoataarifa	Wanaopendekeza Majina ya Lugha za Kigeni	Wanaopendekeza Majina ya Lugha za Asili
Wasukuma	10	7	3
Wabena	10	8	2
Wajita	10	9	1
Wahaya	10	9	1
Wanyakyusa	10	9	1
Wakinga	10	7	3
Wazaramo	10	8	2
Wangindo	10	9	1
Wachaga	10	8	2
Wasambaa	10	7	3
JUMLA	100	81	19
%	100%	81%	19%

**Chanzo:** Uwandani (2019/2020)

Kwa kuchunguza data katika Jedwali Na. 5, ni wazi kwamba watoataarifa 81 waliona hakuna haja ya kutumia majina ya lugha za asili ilhali watoataarifa 19 walionekana kupenda kutumia majina hayo. Matokeo haya yanaonesha kwamba kundi kubwa la vijana waliohusishwa wanaona hakuna umuhimu wa kutumia majina ya lugha zao za asili. Majina ya lugha za kigeni ndiyo yanayoonekana kupewa kipaumbele. Katika mazingira hayo, lugha za kigeni zinaonekana kuwa muhimu na za thamani kuliko lugha za asili. Hoja hii pia iliukiliwa na hali halisi iliyojibainisha uwandani ambapo ilionekana wazi kwamba baadhi ya vijana kutoka katika jamiilugha zilizoteuliwa hawakuweza kuzungumza lugha zao za asili badala yake walitumia lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, halikuwa jambo la kustaajibisha kuona kwamba watoataarifa hao wanathamini lugha za kigeni badala ya lugha zao za asili kwa kuwa hata lugha zenyewe hawakuwa na uwezo wa kuzizungumza. Ni wazi kwamba watoataarifa wameonekana kutokuthamini lugha zao za asili ambazo ni sehemu ya utamaduni wao. Hivyo basi, utambulisho wa jamii husika unadhoofishwa, na amali za jamii husika haziwezi kudumishwa na kulindwa kama inavyopaswa kwa vizazi vijavyo. Matokeo haya yanaendana na Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu kwa kuwa inaonekana kwamba lugha za kigeni zinakandamiza lugha za kiasili na jamii inaona fahari kutumia majina ya lugha za kigeni kuliko majina ya asili, suala linaloshadidiwa na mhimili wa mitazamo katika nadharia hiyo.

Hata hivyo, ifahamikie kwamba masuala yanayochochea matumizi ya lugha fulani katika jamii, hususani za kigeni, ni pamoja na athari za ukoloni ambapo hutokana na nguvu za kiuchumi, kiteknolojia, kijamii na kisiasa za mataifa ya kigeni. Hivyo, lugha za mataifa hayo hupewa thamani katika mataifa yasiyo na nguvu hizo. Hatimaye, jamii isiyo na nguvu huamua kutumia lugha za mataifa yenye nguvu kwa kudhani kwamba itanufaika kiuchumi, kisiasa na kadhalika (Giles na Byrne, 1982). Licha ya ukweli kwamba mataifa ya Afrika yako huru, bado tunahitaji kutafakari vizuri kuhusu uhuru wa kifikra hususani kuhusu mila na desturi za Mwafrika pamoja na tamaduni ambapo lugha zetu ni sehemu ya tamaduni hizo.

### 8.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza kipengele cha uteuzi wa majina ya watu kwa lengo la kubainisha kiwango cha matumizi ya majina ya lugha za kigeni, suala ambalo lilidokezwa katika tafiti za awali bila kushadidiwa na data mwafaka. Matokeo ya data zilizokusanywa yanaonesha kwamba matumizi ya majina ya lugha za kigeni ni ya jumla ya asilimia 77 ambapo majina ya lugha za asili yamebainika kutumika kwa asilimia 22. Kwa upande wa changamoto zinazotokana na matumizi ya majina ya lugha za kigeni, imebainika kwamba kuna ugumu katika kutamka baadhi ya majina ya lugha za kigeni na baadhi ya majina hayo yana makosa ya kitahaja. Zaidi ya hayo, baadhi ya majina ya lugha za kigeni yameonekana kujidhihirisha katika umbo zaidi ya moja. Aidha, imeonekana kwamba matumizi ya majina ya lugha za kigeni husababisha kupotea kwa dhima ya utambulisho kutokana na majina na huzifanya lugha za kigeni kuthaminiwa ilhali lugha za asili zikiendelea kupoteza hadhi yake na historia ya jamiilugha husika. Kwa upande wa mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya majina ya lugha za kigeni, imebainika kwamba kati ya vijana 100 waliosailiwa, 81 wameonekana kupendelea majina ya lugha za kigeni wakati watoatarifa 19 wakipendelea kutumia majina ya lugha ya kiasili.

Kwa ujumla, lugha za kigeni zimeonekana kukandamiza lugha za kiasili na jamii inaonekana kuwa na mtazamo kwamba majina hayo ndiyo yenye hadhi na yanayofaa zaidi kuliko majina ya lugha za kiasili. Hivyo basi, Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu imeakisiwa vyema katika uchanganuzi wa data za makala hii.

### Marejeleo

- Anthony, H. (2021). Uchunguzi wa Maana na Vipengele vya Kiisimujamii Vinavyoukilia Uteuzi wa Majina ya Kiswahili ya Dawa za Asili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Buberwa, A. (2017). "Kiswahili Personal Names Selection in Tanzania: A Sociolinguistic Analysis." *Kiswahili*. 80:21-31.
- Buberwa, A. (2018). "Sexism in Haya Language Personal Names Selection." *JULACE*. 3(2): 111-126.

- Carpusor, A.G. na Loges, W.E. (2006). "Rental Discrimination and Ethnicity in Name." *Journal of Applied Social Psychology*. 36 (4): 934-952.
- Gary, G. na Mahoney, J. (2012). *Qualitative and Quantitative Research in Social Science*. United Kingdom: Princeton University Press.
- Giles, H. (1979). "Ethnicity Markers in Speech." Katika K.R. Scheres na H. Giles (Wah.), *Social Markers in Speech*. Kur. 251-289.
- Giles, H. na Byrne, J.L. (1982). An International Approach to Second Language Acquisition. *Journal of Multilingual and Multicultural Development*. 3:19, 17-40.
- Kimbwanda, F.M. (2021). Kiwango cha Matumizi ya Majina ya Watu ya Lugha za Asili katika Jamii ya Wangindo: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Kiswahili na Kingindo. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Lusekelo, A. na Mtenga, V. (2020). "Historicity of Personal Names in Tanzania: The Case of the Names in the Rombo-Chaga Community in Kilimanjaro." *International Journal of Modern Anthropology*, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Madila, Z. (2020). Matumizi ya Majina ya Kiswahili Jijini Dar es Salaam, Nchini Tanzania: Uchunguzi Kifani wa Majina ya Watu. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Msanjila, Y.P., Kihore, Y.M. na Massamba, D.P.B. (2009). *Isimujamii: Sekondari na Vyuho*. Dar es Salaam: TUKI.
- Nyangaywa, M. (2013). Uchunguzi wa Semantiki na Taratibu za Utoaji wa Majina ya Kijita. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Phillipson, R. (1992). *Linguistic Imperialism*. Oxford: Oxford University Press.
- Rubanza, Y.I. (2000). "The Linguistic Creativity of Haya Personal Names." *Kiswahili*. 63:11-22.
- Tabouret-Keller, A. (1989). *Seminar Danthropologic du language*. MSH Informations. Bulletin de la Fondation des Sciences de l'Homme NO. 59: 15-17.